**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

***Andika insha itakayoanza kwa:***

*Nilipomtazama ndugu yangu kwa mara ya kwanza tangu kuachiliwa na watekanyara machozi ya furaha yalinitiririka*.............................................................................................................................

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Umaskini wa nchi___1___vijana kwa wazee kutamani na___2___ njia za mikato za ___3___. Wahusika hufanya___4___ kutafuta mianya ya___5___ fedha. Wao hufanya haya___6___ kujali madhara___7___ na vitendo vyao. Watu huzidi ___8___ ili kuficha maovu haya. Ufisadi___9 uchumi wa nchi kudidimia.

1. **A.** umewatenda **B.** umewafanya **C.** imewafanya **D.** wamewafanya
2. **A.** kuelekea **B.** kufuata **C.** kutenda **D.** kuzifuata
3. **A.** kuwatajirisha **B.** kutajirika **C.** kujitajirisha **D.** kujifilisisha
4. **A.** juu chini **B.** dhahiri shahiri **C.** jino na ukucha **D.** usiku na mchana
5. **A.** kujielekezea **B.** kujipenyezea **C.** kufuja **D.** kujiondolea
6. **A.** mighairi ya **B.** licha ya **C.** ingawa **D.** mradi
7. **A.** zinazoletwa **B.** yanaletwa **C.** yaletwayo **D.** yaletwao
8. **A.** kuzunguka mbuyu **B.** kula mwata **C.** kula mwande **D.** kupasua mbarika
9. **A.** ukitokomea **B.** ukikita **C.** ukikithiri **D.** ukikirihi

Mweledi alipoanza ___10___ kiswahili aligundua kuwa sauti ni muhimu katika mawasiliano. Alitambua sauti ghuna kama vile___11___ na kuzichangamkia. Akawa mwepesi wa kuyakiri mashairi kama vile ___12___ yaani yaliyo na mishororo mitano kwa kila ubeti. Sio hayo tu ___13___ alijifunza methali kama vile ___14___. Hii ni methali___15___ inatuhimiza kuwathamini wenzetu kwani huenda wakatufaa baadaye.

10. **A.** kufunza **B.** kufunzwa **C.** kusoma **D.** kujifunza
11. **A.** b, dh, g. **B.** f, h, v. **C.** s, t, b. **D.** j, f, th.
12. **A.** tarbia **B.** takhmisa **C.** ngonjera **D.** utenzi
13. **A.** mbali pia **B.** aidha labda **C.** bali pia **D.** japo tena
14. **A.** baniani mbaya kiatu chake dawa
    **B.** cheche za moto huchoma msitu
    **C.** afadhali dooteni kama ambari kutanda
    **D.** usikate ubeleko kabla mtoto hajazaliwa
15. **A.** ambao **B.** ambawo **C.** ambayo **D.** a[illegible]aye

**16.** **Chagua kielezi katika sentensi ifuatayo:**

*Mchezaji mahiri na mnyenyekevu aghalabu huwafurahisha mashabiki wengi.*

A. mahiri

B. aghalabu

C. mnyenyekevu

D. wengi

**17.** **Chagua wingi wa:**

*Hukufahamu kuwa timu yangu ingekupatia ushindi shindanoni?*

A. Hawakufahamu kuwa timu zetu zingewapatia ushindi mashindanoni

B. Hamkufahamu kuwa timu zetu zingewapatia ushindi mashindanoni

C. Hamkufahamu kuwa timu zangu zingewapatia ushindi mashindanoni

D. Hamkufahamu kuwa timu zetu zingempatia ushindi mashindanoni

**18.** **Ukubwa wa sentensi:**

*'Kidole kifupi kina ukucha mrefu,'* ni

A. Dole fupi lina kucha refu

B. Vidole vifupi vina kucha ndefu

C. Dole fupi lina makucha marefu

D. Vidole vifupi vina makucha virefu

**19.** Ni sentensi ipi yenye kivumishi halisi?

A. Shamba hili ni pana kuliko lile jingine

B. Dawati zuri la kupendeza limeuzwa

C. Taifa linahitaji vijana wengi kuimarika kiuchumi

D. Kijana mpole atatuzwa na mwalimu wake

**20.** Neno , **'ghadhabishwa'** lina herufi ngapi za alphabeti ya kiswahili?

A. Kumi na mbili

B. Nne

C. Nane

D. Tisa

**21.** Chagua nomino iliyoundwa kutokana na nomino

A. Mbio - kimbia

B. Kicheko - ucheshi

C. Nyamaza - Nyamavu

D. Tamu - utamu

**22.** Neno, **'Karibu'** limetumikaje katika sentensi:

*Ameteleza karibu aanguke matopeni.*

A. Makaribisho

B. Kiasi

C. Nusura

D. Wakati

**23.** Subui nne kwa tarakimu huandikwaje?

A. $\frac{4}{6}$

B. $\frac{4}{9}$

C. $\frac{7}{4}$

D. $\frac{4}{7}$

**24.** Kauli zilizopigiwa mstari zimetumia tamathali gani za usemi?

<u>*Kenga ni ninga anaimba kama malaika.*</u>

A. Majazi, nahau
B. Tasfida, kinaya
C. Sitiara, tashbihi
D. Tashbihi, nahau

**25.** Usemi taarifa wa, "*Nimechoka, nataka kupumzika,*" mfanyakazi alituambia.

A. Mfanyakazi alituambia kuwa amechoka na alitaka kupumzika.
B. Mfanyakazi aliwaambia kuwa alikuwa amechoka na alitaka kupumzika.
C. Mfanyakazi aliwaambia kuwa angechoka na angetaka kupumzika
D. Mfanyakazi aliwaambia kuwa alikuwa amechoka na angetaka kupumzika.

**26.** Chagua jibu lisilolingana na mengine:

A. Kubali - kataa
B. Umba - umbua
C. Kubali - lidhia
D. Kusanya - tawanya

**27.** **Tegua kitendawili:**

*Nitembeapo yupo, nikimbiapo yupo niingiapo ndani hayuko.*

A. Kivuli
B. Upepo
C. Mwangaza
D. mwangwi

**28.** Chagua maana ya methali:

Chovya chovya humaliza buyu la asali

A. Ukijiwekea akiba kidogo kidogo hatimaye utapata donge nono
B. Ukitumia akiba yako kidogo kidogo mwishowe itamalizika
C. Ukifuja mali yako kidogo kidogo hatimaye yataongezeka
D. Ukitia kidole kidogo kidogo hatimaye yataongezeka

**29.** Kipeto ni cha mawele au maharagwe au ngano pia kipeto ni cha

A. mzabibu
B. mpingo
C. mtama
D. mbuyu

**30.** Kiangazamacho ni zawadi anayopewa mtu kwa kuokota kitu kilichopotea. Ridhaa ni

A. malipo kwa ajili ya kuvunjiwa heshima
B. Pesa za matumizi ya kila siku
C. malipo ya kumsajili mtoto shuleni
D. malipo kwa kumtoa mtu damu

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Kandanda ni miongoni mwa michezo maarufu kote duniani. Wafuasi wa mchezo huu wamesambaa dunia nzima. Wafuasi hawa huitwa mashabiki. Katika kila nchi mashabiki huwa na timu zao hususan katika miji yao. Aghalabu timu hizi huchukua majina ya miji husika. mashabiki hawa ni wa kila tabaka. Walivyo navyo na wasiokuwa navyo. Kuzungumza kinyume cha timu yao ni kama kukasiri nguo na itikadi zao. Zogo huweza kuzuka kwa sababu ya swala hili. Timu zinapogaragazana, mashabiki hawawezi hata kujikinga kutokana na mvua. Badala ya kujibari, wao husimama kidete wakishangilia kwa vifijo na nderemo.

Chimbuko la mchezo huu halijulikani kabisa ila inaaminika ulianzia Japani na Uchina. Baadaye ulipelekwa Uingereza na Warumi walipoitawala kabla ya kuzaliwa kwa kristo. Enzi hizo, mchezo huu ulitumiwa kuwatumbuiza wafalme, malkia na watu wengine matajiri. Mchezo huu ulichezwa kwa miguu peke yake ila siku hizi huchezwa kwa kila sehemu ya mwili isipokuwa mikono.

Zama hizo, mchezo huu ulikuwa ukichezwa baina ya vijiji. Kijiji kimoja kiliunda timu na kucheza dhidi ya kingine. Inasemekana kuwa kiliunda timu na kucheza dhidi ya vijiji. .Inasemekana kuwa mechi moja ingechukua takriban siku tatu kukamilika. Milingoti ya magoli ilikuwa mita chache hadi kilomita chache kutoka kwa nyingine. Vita viliweza kutokea baina ya timu hizo za wanavijiji. **Kuusukuma mpira hadi** kufika mbali kulihitaji maarifa ya wanaume wa [illegible]. Kengele [illegible] kuwajulisha mashabiki kuwa [illegible] wamefunga bao. Labda kilomita tatu kutoka walipokuwa. Kwa madhumuni ya kupunguza utumiaji wa nguvu kwa kucheza shelabela, mpango mahususi ulibuniwa wa kutoa pasi kwa mwenzako katika sehemu nyingine ya uwanja. Kiwango cha wachezaji kilipunguzwa kutoka ishirini na saba hadi kumi na mmoja. Masafa nayo walipunguzwa kutoka sita. Mchezo wa kisasa chimbuko lake ni uingereza baada ya sheria zake kuandikwa [illegible] marekebisho ya hapa na pale.

Mchezo huu unakusudiwa [illegible] na manufaa yakiwemo kuimarisha afya ya mwili, kujichangamsha, kutoa mazoezi ya akili kwa kuchangamsha ubongo, wasemavyo wayunani kuwa akili timamu hukaa katika mwili wenye afya. Mchezo huu umekuwa njia mojawapo ya watu kujipatia riziki. Wachezaji hulipa kiasi kikubwa cha darahimu. Ushindi unasudiwa sana. Mshindi huondoka uwanjani na kisasi akingojea muda mahususi wa kulipiza. Jambo hili ndilo huzua vurumai miongoni mwa mashabiki hasa wakipokezwa kichapo kingine. Kujipatia umahiri katika mchezo huu si jambo la kujikalia tu. Kazi ipo. Ukibahatika wimbo wako hautadidimia na sifa zako zitaenea hadi utakapofumwa na mvi wa manaya.

Kutunukiwa kombe kwa mshindi ni jambo la tangu jadi. Kinaya ni kuwa mshindi alikarpiwa na kusomewa na hata kupigwa kwa mayai yaliyooza. Kama ilivyo michezo mingine, kandanda hutawaliwa na sheria. Sheria hizo lazima zifuatwe na marefarii ili kuhakikisha kuwa haki imetendeka uwanjani. Wachezaji hufanya mazoei kabla ya kuanza kufanya mchezo. Mchezo huu kwa kawaida unahitaji watu kufanya kazi kwa pamoja ili kujipatia ushindi.

31. Kulingana na aya ya kwanza
A. kandanda ni mchezo maarufu kote duniani
B. mashabiki wa kandanda hupatikana kila kijiji
C. kila mji huwa na timu ya kandanda
D. mashabiki hushangilia timu zao kwa uzalendo.

32. Aya ya kwanza inaonyesha kuwa
A. kuzuka kwa vurumai wakati wa mchuano ni jambo la kawaida
B. mashabiki hawalowi wanaponyeshewa na mvua
C. shabiki anaweza kujitolea kwa hali na mali kushangilia timu yake
D. kandanda huwa na mashabiki kutoka matabaka yote ya kijamii

33. Kulingana na aya ya pili
A. asili ya mchezo wa kandanda ni Uchina na Japani
B. walindalango hutumia sehemu zote za mwili wanapocheza
C. sehemu zote za mwili hutumiwa unapocheza kandanda
D. Warumi walianza kucheza kandanda kabla ya kuzaliwa kwa kristo.

34. Mwandishi anaeleza kuwa zamani;
A. mechi ingechukua siku tatu kukamilika.
B. mechi ingechukua zaidi ya siku tatu kukamilika
C. mechi ingechukua karibu siku tatu kukamilika
D. kandanda ingechukua dakika tisini kukamilika

35. Kwa mujibu wa taarifa, jibu linalodhihirisha maana ya methali:
*"Kichango ni kuchangizana,"* ni
A. wachezaji kushirikiana kwenye mechi ili kupata ushindi.
B. mashabiki kuzua vurumai uwanjani wanapotofautiana
C. kandanda kuchezwa kati ya kijiji kimoja na kingine
D. Marefarii kutumia sheria kufanya maamuzi ya haki.

36. Kifungu kimebainisha kuwa:
A. Kandanda inahitaji bidii wala si uzembe
B. Timu hulipiza kisasi kwa nyingine kwa kuzua vita
C. Mshindi hufurahia anapoondoka uwanjani
D. Ushindi katika kandanda hauthaminiwi

37. Maana ya, *"Akili timamu hukaa katika mwili wenye afya,"* ni
A. mtu anayeugua hana akili timamu
B. afya ya ubongo huhitaji mazoezi
C. ubongo ukichangamshwa kwa mazoezi hufanya kazi ifaavyo
D. afya ya mwili inahitaji akili timamu

38. Kwa nini wachezaji wa kandanda wa kale walihitaji kuwa wanaume wa miraba minne?
A. Mechi zilichukua muda mrefu kukamilika
B. Kila timu ilitaka kuibuka na ushindi
C. Idadi ya wachezaji ilikuwa kubwa sana
D. Eneo la kuchezea lilikuwa kubwa sana.

39. Ni jambo gani ambalo timu iliyoshindwa haikufanyiwa?
A. Kukaripiwa
B. Kupokezwa tuzo
C. Kupigwa kwa mayai yaliyooza
D. Kusomewa na mashabiki

40. Funzo kuu tunalopata kutokana na kifungu hiki ni kuwa:
A. Mchezo wa kandanda umepitia mabadiliko makubwa
B. Kandanda ni mchezo wenye manufaa mengi
C. Kufanikiwa katika mchezo wa kandanda kunahitaji ushirikiano
D. Visa vya utovu wa nidhamu wakati wa mechi vinaepukika.

Compiled & Distributed by Schools Net Kenya P.O. BOX 15509-00503, Nairobi
Tel 0734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50***

Japo wazazi wa Hamisi walimpeleka shuleni, hawakuwa na matumaini naye. Waliona kana kwamba walitupa pesa na mali yao kwenye biwi la moto. Hamisi alikuwa na ulemavu wa kutamausha. Hata hivyo, wazazi wake hawakuchoka kumpatia mahitaji yote na mapenzi aliyohitaji. Hali hii ilikuwa kinyume na hapo awali ambapo walimficha ili asionwe na watu hasa waliozaa watoto wasiokuwa na ulemavu. Baada ya ushauri kutoka kwa mshauri nasaha, walibadili nia na kudhihirisha mapenzi ya dhati kwa mwanao.

Ficha ficha hii ilisababisha Hamisi kuanza masomo akiwa na umri mkubwa. Hamisi alikumbana na changamoto tele. Kutokana na ulemavu wa mkono, aliandika kwa shida. Ulemavu wa miguu uliathiri mwendo wake. Hata hivyo, maji ukiyavulia nguo sharti uyaoge. Alijizatiti masomoni. Alijizoesha kuandika kwa mkono alioumbiwa na Mola wake. Kumbe Mungu hukupa ulemavu na mwendowe.

Licha ya ulemavu wake, baadhi ya wanafunzi wasiokuwa na ulemavu wa mwili walimpenda na wengine walimponza kwa kiburi. Wapo waliomwona kama mbwa na hata wengine walishangaa iwapo angepata mchumba maishani. Wengine walimkejeli na hata waliomwambaa. Hata hivyo, hakuwa na kinyongo na yeyote. Hakulipa mabaya kwa mabaya. Lakini hata kuna mahasimu wake walipotaka msaada aliwaauni. Licha ya ulemavu, alijaliwa na hati nzuri na kipawa cha uchoraji. Akawa bingwa na hati nzuri na kipawa cha uchoraji. Akawa bingwa na kuchora mahasibu wake waliajabia kazi yake ya sanaa. Muda haukupita kabla kuanza **kujizumbulia riziki** japo kidogo. Kwa kweli, ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.

Wazazi wake walianza kujiuma vidole ni kwa nini walilimatia kumpeleka mwanao shule kwa kuhofia soni. Lile hawakufahamu ni kuwa mficha uchi hazai. Walimu na wanafunzi nao walianza kufurahishwa na makala mengi aliyoyandika kwa ubunifu mkubwa na ukwasi wa lugha.

Ingawa Hamisi alipenda soka, hakuwa na uwezo mkubwa wa kuisakata. Badala yake akaibukia kuwa shabiki sugu. Jumamosi moja alikata shauri kujikokota hadi uga wa michezo kushuhudia mechi ya soka. Mechi ilipokamilika kama kawaida, washindi walishangilia kwa shangwe na nderemo. Ghafla vurumai ikatokea. Hamisi alikuwa amefika barabarani akirejea kwao.

Kundi moja la wahuni lilimwinua juu juu na kumwachilia. Akaanguka kando ya barabara. Akagaragara kwa machungu bila usaidizi. Ikawagharimu mkono wa wasamaria wema kumnusuru na kumkimbiza hospitalini. Hospitalini , alitakiwa kueleza, mwanahabari mmoja kilichojiri. Alipokuwa akieleza, mwanahabari mmoja aligundua kuwa Hamisi alikuwa na sauti ya kipekee. Baadhi ya zile walizokuwa wakisaka. Baada ya kupona Hamisi alijikuta katika idhaa ya kiswahili ya jipe raha. Hata waliokuwa wakimbeza na kumdharau kutokana na ulemavu wake, walianza kumpa nyama ya ulimi. Kumbe akitupwa majini hafi.

41. Kulingana na aya ya kwanza:
A. Hamisi hakupelekwa shuleni
B. Ulemavu wa Hamisi ulitamausha
C. Mwanzoni Hamisi hakutangamana na watoto wenzake
D. Hamisi alitangamana na watoto walemavu pekee hapo awali

42. Kifungu kimebainisha kuwa wazazi wa Hamisi hawakutaka kumpeleka shuleni kwa kuwa:
A. Waliona haya kutokana na ulemavu wake
B. Hamisi alikuwa mtoto mlemavu
C. Watoto wasiokuwa na ulemavu walimchukia
D. Angepata changa moto nyingi shuleni

43. Chagua jawabu linaloonyesha kuwa Hamisi alibaguliwa
A. kutoruhusiwa na wazazi kutangamana na wanafunzi, kumtania kupendwa na wanafunzi wachache
B. kuumizwa na mashabiki, kunyimwa haki ya masomo na kutoruhusiwa na wazazi kutangamana
C. kupelekwa hospitalini na wasamaria, kutaniwa na wanafunzi na kunyimwa haki ya masomo mwanzoni
D. kunyimwa haki ya masomo, kutoruhusiwa kutangamana, kubezwa na wanafunzi.

44. Kifungu kimebainisha kuwa Hamisi alikuwa na vipaji vifuatavyo isipokuwa:
A. Sauti ya utangazaji
B. Kuchora
C. Mwandiko mzuri
D. Kucheza soka

45. Neno, **'aliwaauni,'** limetumika kwenye kifungu. Maana yake ni
A. aliwasaidia
B. aliwapatia
C. aliwashangaza
D. aliwaogopa

46. Chagua jawabu lisilo sahihi kwa mujibu wa kifungu.
A. Wazazi wa Hamisi walijuta kutompeleka shuleni kutokana na aibu
B. Mahasidi wa Hamisi shuleni walichukia michoro yake.
C. Ushauri kwa wazazi ulichangia Hamisi kupelekwa shuleni
D. Ulemavu wa Hamisi hakuathiri talanta zake

47. **"Chura akitupwa majini hafi,** dhihirisha jinsi methali hii inavyoafiki Hamisi.
A. Hamisi alipendwa na baadhi ya wanafunzi wasiokuwa na ulemavu
B. Hamisi kutumbukia kwenye vurumai na kuumizwa
C. Hamisi anapoumizwa na kutupwa kando ya barabara na kulazwa ndipo talanta yake inapobainika
D. Hamisi kuibuka bingwa wa kuchora na kipawa chake kuanza kumpa riziki ndogo ndogo.

48. *"Hata waliokuwa wakimbeza na kumdharau kutokana na ulemavu walianza kumpa nyama ya ulimi."*
Chagua tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika kauli hii
A. tashbihi, sitiari
B. ishara, tashhisi
C. chuku, majazi
D. kinaya, nahau

49. Kulingana na kifungu, Hamisi hakuwa na kinyongo kwa kuwa
A. aliwasaidia hata maadui zake
B. hakulipa ubaya kwa ubaya
C. aliheshimu wazazi wake licha ya kutomshughulikia mwanzoni
D. aliwasamehe waliomsababishia majeraha barabarani.

50. Maana ya kujizumbulia riziki ni
A. kujipatia mapato
B. kujulikana na wengi
C. kuwa maarufu
D. kujipatia mahitaji muhimu